## UFUGAJI WA KIENYEJI WA BATA BUKINI



Bata Bukini ni ndege ambao asili yao ni India na Japan. Hii ni jamii ya ndege wafugwao lakini tofauti kubwa ya bata wa kawaida wao wana asili ya usafi, hivyo hawapendi uchafu na kamwe hawali mizoga.

**Banda**

Bata Bukini wanahitaji nafasi ya kutosha hivyo andaa banda kulingana na wingi wa bata unaotarajia kufuga.

Hakikisha banda limesakafiwa au banda la udongo lisilotuamisha maji au unaweza kuweka mbao au mabanzi kisha unaweka maranda ili kuwakinga na baridi.

**Chakula**

Ndege hawa wanakula chakula kama wanacholishwa kuku, wanapendelea kula majani jamii ya mikunde kwa 50% na hawahitaji chakula kingi. Vifaranga ni lazima wapatiwe lishe kamili hasa protini kwa wingi ili waweze kujenga mwili, kukua vizuri na kuwa na afya nzuri.

**Mahitaji**

- Chokaa kilo 5 (ya kulishia mifugo)
- Mashudu kilo 20.
- Dagaa kilo 10 (wanaotumika kulishia kuku)
- Mahindi kilo 10 ( hakikisha hayana dawa)

**Utengenezaji na Uhifadhi**

Baada ya kupima vyakula hivi kwa usahihi chukua pipa, changanya vizuri kisha walishe bata kulingana na wingi wao na uhakikishe wanapata chakula cha kutosha.Vipimo hivi hutegemea wingi wa bata unaowafuga lakini hakikisha uwiano huo unazingatiwa. Baada ya kutengeneza chakula unaweza kuhifadhi katika mifuko na kuweka katika eneo lisilokuwa na unyevu.

**Kuatamia**

**Jinsi ilivyotofauti katika idadi ya utagaji wa mayai hivyo ndivyo uwezo wa kuatamia pia ulivyo. Bata Bukini weupe huatamia mayai 6 na wale wa rangi huatamia mayai 12**

Ndege hawa huatamia kwa siku 29, huangua vifaranga kwa siku 3 na mara nyingi hutotoa mayai yote, si rahisi mayai kubaki bila kutotolewa au kuharibika.

**Namna ya kutunza vifaranga**
Mara tu vifaranga wanapoanguliwa, wachukue na kuwatenga na mama yao kisha waweke katika banda safi lisilopitisha baridi. Unaweza kuwawekea taa ya umeme kama una uwezo ili kuwatengenezea joto.

Pia, waweza kuzungushia banda lao kitu kizito kama blanketi ili kuwakinga na baridi au upepo.

**Maji**

**Ni lazima bata wapatiwe maji ya kunywa kila siku na hakikisha banda halikosi maji wakati wote. Safisha chombo cha maji na kubadilisha maji kila siku.**
Ndege hawa wanahitaji maji ya kunywa ya kutosha kama ilivyo kwa kuku. Hakikisha maji yako kwenye chombo ambacho hayatamwagika , kwani kumwagika kunaweza kusababisha kuibuka kwa magonjwa. Bata Bukini hawapendi uchafu. Hivyo maji yawe mahali ambapo hayatachafuka.

**Magonjwa**
Ni mara chache sana bata bukini kushambuliwa na magonjwa kama watawekwa katika hali ya usafi. Magonjwa yanayoweza kuwasumbua ni mafua na wakati mwingine kuharisha.

**Tiba za asili**

Unaweza kutibu bata bukini kwa njia za asili. Tumia mwarobaini, vitunguu (maji na saumu).

**Mwarobaini**
Unaweza kutumia dawa hii kutibu mafua kwa bata bukini wakubwa au vifaranga

**Maandalizi**
Chukua kiasi kidogo cha mwarobaini kisha twanga vizuri kupata maji maji. Kamua maji ya mwarobaini, kisha changanya na maji uliyo andaa kuwanywesha vifaranga.

**Kitunguu Saumu na Kitunguu Maji**:
Dawa hii hutumika kukinga na kutibu bata bukini wanaoharisha.

**Maandalizi**
Unachukua kitunguu saumu au maji na kuondoa maganda ya nje kisha safisha na kukata vipande vidogovidogo na kuwawekea kama chakula.Unaweza kuwapatia kila siku hadi watakapopona.

Imetolewa: [http://kilimohaitz.blogspot.com/2018/07/ufugaji-wa-kienyeji-wa-bata-bukini.html](http://kilimohaitz.blogspot.com/2018/07/ufugaji-wa-kienyeji-wa-bata-bukini.html)

01/10/2018